TANGAZO LA SERIKALI Na. 75 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MBAGALA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mbagara ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Mafinga.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya ya mpaka ya upimaji namba HMU 49 yenye maira - nukta 752751.000MS, 9084253.791KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.61 hadi kwenye makutano ya mto Kinyapera kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBL 01 yenye majira - nukta 753357MS, 9084343KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mto Kinyapera kwa umbali wa kilomita 1.93 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBL 02 yenye majira - nukta 752306MS, 9083535KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.42 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBL 03 yenye majira - nukta 752477MS, 9083922KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.22 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMT 894 yenye majira - nukta 752688.879MS, 9083877.579KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.26 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMT 918 yenye majira - nukta 752751.000MS, 9084129.944KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMU49 hadi ulipoanzia''

Dodoma,
………., 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*